


# MAPINDUZI YA KIJANI AFRIKA

## NI NINI?



duducoelho.com

**M**apinduzi ya kijani yanamaanisha maendeleo ya aina za mbegu zinazozaa kwa wingi, ambazo pia hujulikana kama mbegu zilizoboreshwu au 'mbegu zilizothibitishwa'. Aina hizi za mbegu zimezalishwa maalum kwa ajili ya kuongeza uzalishaji kwa hekta, kama sehemu ya kifurushi cha teknolojia (ufundi) kinacho jumuisha mbolea zisizokuwa za kilimo hai, viuatilifu na pembejeo nyingine za kemikali, uvezeshwaji wa kifedha, uhakika wa masoko ya bidhaa n.k.

Watetezi wa Mapinduzi ya Kijani wana hoja kwamba taratibu zake zinahamasisha vizuri zaidi uendelevu

wa kilimo, na uhakika wa chakula na lishe. Mantiki yao ni kwamba wakulima watanunua pembejeo (ambazo zinaweza kupata ruzuku kwa misimu michache ya mwanzoni ili kuanzisha mchakato), ambao utawawezesha wao kupata mavuno zaidi ambayo yanaweza kuuzwa kwa faida. Matokeo yake ni kuzalisha kipato cha kutosha kununua mahitaji ya chakula mpaka msimu mwagine na kununua pembejeo kwa uzalishaji zaidi.

Uhalisia ni kwamba, haifanyi kazi hivyo, na ni sehemu ndogo tu ya wakulima ndiyo inayoweza kufaidika kwa utaratibu huu.

